JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

HALI YA UCHUMI DUNIANI SASA SHWARI, WATUNGA SERA WA AMSHWA

"Embu nianze na habari njema,Uchumi wa Dunia umerudi katika hali yake ya kawaida zaidi ya tulivyotegemea.Ninafuraha kuwajulisha hivyo na ni muhimu kuifahamisha Dunia".Haya yamesemwa na Mshauri wa Uchumi wa Shirika la
Fedha la Kimataifa (IMF) na Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti Bw. Olivier Blanchard alipokuwa akiongea na waandishi wa habari mjini Washington DC."Hii ni habari njema sana", alisisitiza huku akiwa na furaha tele.

Bw. Blanchard alieleza kuwa Sasa tunategemea uchumi kukua hadi kufikia asilimia 4.2 kwa mwaka 2010, ambapo itakuwa imepanda kwa asilimia 3 kutoka kwenye makadirio yetu ya mwezi January na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2011.Mbali na ukuaji huo wa Uchumi , biashara Duniani imeiimarika na mitaji imeendelea kuongezeka.

Aidha aliendelea kueleza kuwa kama tulivyojadiliana katika ripoti ya mambo ya fedha tumeona kuwa hali ya soko la fedha imeendelea kukua na kuimarika. Haya matokeo mazuri yameonekana katika nchi zilizoendelea na zinajionyesha zaidi katika nchi ambazo zinaendelea. Embu sasa nisikilizeni ni waelezee kwa kimakundi " alijigamba Mchumi huyo.

Aliendelea kueleza kuwa tunapoangalia kwenye nchi ambazo uchumi wao ni mkubwa zaidi tunaotea kuwa uchumi utakuwa kwa asilimia 2.3 kwa mwaka 2010, na asilimia 2.4 kwa mwaka 2011, hii tu haitoshi kuziba pengo lililotokea katika kipindi cha mtikisiko. Asilimia 7 imekuwa ni matokeo ya chini ya tofauti iliyopo na tofauti hii inategemewa kuwa kubwa kwa miaka mingi ijayo.

Tofauti hii inasababisha ajira kupungua kwa kiasi kikubwa, lakini tunategemea ukosefu wa ajira katika nchi zenye uchumi mzuri kufikia asilimia 8.4 kwa mwaka 2010 na kupungua kwa asilimia 8 kwa mwaka 2011.

"Nini kilicho sababisha utendaji huo dhaifu na tofauti isiyofikirika? nafikiri ni udhaifu wa mahitaji" . Aliuliza mchumi huyo. Hapa Amerika, walaji, ndio waliokuwa wakiendesha uchumi kabla ya mtikisiko, sasa wamekuwa makini kujua ni nini kinaweza

kutokea.Ulaya, ambakomabenki yanachukua nafasi kubwa ya udalali wa kifedha, sasa hivi sekta hizo zimepunguza utoaji wa mikopo.Huko Japan, ambako kumekuwa na upunguzaji wa ongezeko la fedha sasa wanajitahidi kukabiliana na tatizo hilo.Alisisitiza Blanchard.

Aidha mchumi huyo aliendelea kueleza kuwa ukuaji wa uchumi unategemewa kuwa imara zaidi, kwa asilimia 6.3 kwa mwaka 2010, na asilimia 6.4 kwa mwaka 2011.Bara la Asia linaongoza kwa asilimia 8.7 kwa mwaka 2010, na asilimia 8.6 kwa mwaka 2011. Na uchumi hauonekani tu kuwa imara bali pia kuto yumba kabisa.Sera za kifedha zimesaidia sana kuimarisha uchumi huu na kuufanya usiwe wa kuyumba katika kusimamia shughuli za mwaka 2009 na hata mahitaji binafsi yamekuwa na kufanya uchumi imara na unaoendelea.

Kuimarika kwa uchumi huu kunatufanya tujue changamoto ambazo zinatukabili ili tujipange vizuri katika kuimarisha uchumi wetu na nilazima tuzibe mianya ambayo inaweza kusababisha tatizo hili. Hii inahusu nchi zote zilizoendelea na zinazoendelea. Tusiruhusu tena hali hii kutokea.Alisema Blanchard.

Kwa Nchi zilizoendelea tatizo lilikuwa jinsi ya kuzitumia fedha walizonazo.Na hii ilitokana na utoaji holela wa fedha hasa katika mabeni lakini hili tumeshalifanyia kazi. Alieleza Bw.Blanchard

Kwa hiyo tulichokifanya nikuzuia hiyo mianya na kuweka program ambazo tulijua zitarekebisha hali hiyo na kuongeza fedha pale ambapo palikuwa na mapungufu.

Tunashukuru zoezi hilo lilifanikiwa kwani tulikuwa na wasiwasi sana hasa kwa sehemu zile ambazo ziliathirika zaidi hasa kwa nchi za ulaya kwani haikuwa kazi rahisi. Kwa sehemu ambazo mapato yake yalipungua tulijitahidi kuziba mapengo.Hivyo kwa sasa mambo ya ukusanyaji wa fedha ni shwari na sina wasiwasi.

Blanchard alieleza kuwa Kwa nchi zinazoendelea matatizo yao yalikuwa tofauti, tatizo lao kubwa ilikuwa ni ukosefu wa mitaji mikubwa.Ukuwaji wa uchumi na kuongezeka kwa faida kutoka katika mabenki kunachochea ukuaji wa mitaji.

Mtirirko huo kwetu sisi kwa sasa ni habari njema kwani ndivyo inavyotokea hivi sasa.Lakini tumejifunza kutokana na udhoefu kuwa tunaweza kuvuma na kupasuka.Sasa kitu kikubwa kinachotukabili ni kuwa na sera inayoweza kuhifadhi haya yote kama vile kujua kuwa, ni fedha kiasi gani zinahitajika kiasi kwamba zikikosekana tatizo linaweza kutokea, ni sera gani za uchumi mpana zitumike na ni sera gani za kifedha zitumike, na ni jinsi gani ya kutabiri jinsi hali ya uchumi inavyo kwenda, na ni nyenzo gani zitumike kupambana na janga la kifedha linaloweza kutokea na tutadhibiti vipi kupungua kwa mitaji na kuweka uchumi imara.

Kitu cha kufurahisha na muhimu ni kwamba suluhisho la matatizo haya yaliyozikumba nchi zilizoendelea na zenye uchumi mzuri zinaingiliana na kuungana. Katika uchumi uliokuwa, muungano wa kifedha unahitajika lakini unaweza ukawa na matokeo tofauti katika mahitaji, na katika ukuaji.Ili kuondoa tofauti hizi na kuwa na uchumi unaokuwa ,

nchi zilizoendelea kwa ujumla wake zitahitajika kupunguza thamani za fedha zao ili kuongeza uwiano wa mauzo ya nje.

Hii inamaanisha kwamba nchi zinazoendelea na zilizoendelea kwa pamoja zijiangalie katika sarafu zao ili waweze kufanikisha uuzaji wa mahitaji nje ya nchi zao. Hii ni kwa faida ya wote na kwa kufanya hivi kutazidi kukuza uchumi wa nchi na wa dunia nzima.

Kwa nchi nyingi, inawezekana kufanyika hivyo , kwa mfano China wameondokana na kuuza vitu vya matumizi ya kawaida ili waweze kupunguza akiba zao na fedha zao na hii inakubalika.

Ngoja nimalizie kwa kusema kuwa, tumejikuta tuko katika hatua nyingine ya mpambano na msukosuko.Mdidimio Duniani umetoweka, hali ya uchumi imekuwa nzuri na imekuwa nzuri kuliko tulivyotegemea . Hii kwakweli ni habari inayokaribishika.

Bw. Blanchard alimalizia kwa kusema kuwa upya huu na changamoto hizi hazikuja zenyewe, haikuwa kitu rahisi kabisa kufikia hapa tulipo, hivyo basi, nguvu ya ziada inahitajika kama vile kuwa na fedha za kutosha kwa nchi zilizoendelea , kuwe na marekebisho ya riba na uwiano wa mahitaji duniani kote.Hii ni kazi kubwa inayo wakabili watunga sera kwa miaka michache inayokuja.

Hali hiyo ya mtikisiko wa uchumi uliikumba Dunia takribani miaka mitatu iliyopita

TAARIFA HII IMETOLEWA NA MSEMAJI MKUU
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI
WASHINGTON DC
21/04/2010